

Katika bajeti ya 2009/2010 kwenye mpango wa maendeleo, OWM – TAMISEMI iliidhinishiwa jumla ya **Tshs. 801,000,000/=** kutoka LSRP kwa ajili ya shughuli zinazohusu masuala ya Sheria katika Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Hata hivyo, OWM - TAMISEMI illipokea fedha kiasi cha **Shs. 564,836,000/=** mwishoni mwa robo ya tatu yaani mwezi Machi, 2010 hii ikiwa ni pungufu ya **Shs. 236,164,000/=**

Kwa mujibu wa mpango kazi uliopitishwa na LSRP fedha hizo zitatumika kwa ajili ya shughuli zifuatazo:-

- (i) Kuajiri mtaalamu mshauri kwa ajili ya kuandaa programu ya namna bora ya kuendesha kwa ufanisi Mabaraza ya Kata na Vijiji pamoja na kupitia na kupendekeza marekebisho ya Sheria inayounda Mabaraza ya Kata;
- (ii) Kuendesha mafunzo kwa wadau katika Mamlaka za Serikali za Mitaa ya namna bora ya kuendesha Mabaraza ya Kata;
- (iii) Kufanya mapitio ya Sheria inayounda Mabaraza ya Kata;
- (iv) Kuandaa Mkutano wa Wadau muhimu kupitia programu ya namna bora ya kuendesha kwa ufanisi Mabaraza ya Kata na Mapendekezo ya kurekebisha Sheria inayounda Mabaraza ya Kata;

- (v) Kuendesha mafunzo ya kozi fupi kwa wataalamu wa Idara ya Huduma za Sheria;
- (vi) Kuandaa Mwongozo wa Utekelezaji wa Majukumu ya Askari Polisi Wasaidizi na Mgambo wa Halmashauri bila kuathiri haki za binadamu.

Katika kufanikisha utekelezaji wa shughuli hizi, Idara mpaka sasa imetekeleza mambo yafuatayo:-

- (i) Kuwapeleka watumishi wawili wa Idara kwenye mafunzo ya muda mfupi yanayohusu uandishi wa Sheria na uendeshaji wa mashtaka nchini Swaziland;
- (ii) Kuandaa Rasimu ya Mwongozo wa Utekelezaji wa Majukumu ya Askari Polisi Wasaidizi na mgambo wa Halmashauri bila kuathiri haki za binadamu;
- (iii) Kuajiri Mtaalam Mshauri na kuingia naye mkataba kwa ajili ya kuandaa programu ya namna bora ya kuendesha kwa ufanisi Mabaraza ya Kata na Vijiji pamoja na kupitia na kupendekeza marekebisho ya Sheria inayounda Mabaraza ya Kata.
- (vii) Kuandaa Mkutano wa Wadau muhimu kupitia programu ya namna bora ya kuendesha kwa ufanisi Mabaraza ya Kata na Mapendekezo ya kurekebisha Sheria inayounda Mabaraza ya Kata;